**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 09** **“Amedumaa!”**

**Author** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr. Ngethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**KISUAHELI** **ERIC PONDA**

<table>
<tr><th>Scene</th><th colspan="2">Characters</th><th></th></tr>
<tr><td>1</td><td>1.<br>2.</td><td>SAM<br>CHEMU</td><td rowspan="4">SAM – 17, m.<br>MARIA – 43, f.<br>EDITH – 40, f.<br>EDDI– 36, m.<br>DR SALLY – 34, f.<br>CHEMU – 15, f.<br>NARRATOR</td></tr>
<tr><td>2</td><td>1.<br>2.</td><td>SAM<br>CHEMU</td></tr>
<tr><td>3</td><td>1.<br>2.<br>3.</td><td>SAM<br>CHEMU<br>EDDI</td></tr>
<tr><td>4</td><td>1.<br>2.</td><td>SAM<br>CHEMU</td></tr>
</table>

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** HUJAMBO NA KARIBU KWA SEHEMU YA TISA KWENYE MFULULIZO WA VIPINDI VYETU VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO TUKIWA BADO TUNAZUNGUMZIA MASUALA YA USAFI NA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA KUHARA.KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA SAM NA CHEMU WALITIWA WASIWASI NA HALI MBAYA YA MISALA YAO SHULENI. VYOO HIVYO VIMEJAWA NA NZI NA VILIKUWA VICHAFU SANA.BAADA YA KUPATA USHAURI WA MJOMBA EDDI AMBAYE NI AFISA WA HUDUMA ZA AFYA YA JAMII, USAFI WA VYOO HIVYO UMEIMARISHWA KWA KUYAFINIKA MASHIMO ;KUSAFISHWA KILA WAKATI PAMOJA NA SAKAFU KUNYUNYIZIWA JIVU .HATUA HIZO ZINAUPUNGUZA AU KUUMALIZA KABISA UWEZEKANO WA KUENEA UGONJWA WA KUHARA UNAOSABABISHWA NA VIDUDU AU VIMELEA..

SAM NA CHEMU WAMEJIFUNZA MENGI NA WAMEITUMIA ELIMU HIYO KUUIMARISHA USAFI KATIKA JAMII. JEE KUNA MENGINE YA KUJIFUNZA?.

HEBU TEGA SIKIO MSIKILIZAJI.

**SCENE 1: MARIA'S HOME COMPOUND**

**02. *SFX: FAST FOOT STEPS***

**03. SAM** ***(shouting)*** Chemu… Chemu….Uko ndani? Uko nyumbani ?

**SILENCE**

**04. SAM** Chemu! Chemu! Najua umejificha hapa ndani..

**05. *SFX: DOOR CREEKS OPEN.***

**06. SAM** Chemu, uko wapi?

**07. CHEMU** ***(from a bit far)*** Ssssh….. Usiongee kwa sauti kubwa!

**08. SAM** Kwanini? Kwanini hunijibu?

**09. CHEMU** Ssssh…Nyamaza .. niko hapa chumbani kwa mamangu…!

**10. *SFX: DOOR CREAKS OPEN SLOWLY.***

**11. CHEMU** ***(hissing)*** Kimya .. utamuamsha mtoto…!.

**12. SAM** ***(loud whisper)*** Ohh, sikujua kwamba unashinda tena na mtoto wa jirani…!

**13. CHEMU** ***(loud whisper)*** Umesahau kwamba leo ni siku ya mamake ya kuenda sokoni nami nashinda naye mchana kutwa**.**

**14. SAM** Samahani nilikuwa nimesahau***. (PAUSE.)*** Umesema huyu mtoto ana umri gani?

**15. CHEMU** Kwanza kabisa anaitwa Kwaku..!. Ana umri wa miaka 8. Hebu tutoke hapa kabla ya kumuamsha. Imenichukua muda kumbembeleza mpaka akalala…. Na ni kama sungura…!.

**16. SAM** Sungura....?

**17. CHEMU** **Ana usingizi mwepesi**. Anaamka kila wakati na kuanza kujikuna kuna … tazama..ana mabaka mabaka kote mwilini.

**18.** ***SFX: DOOR OPENS AND SHUTS***

**19. SAM** Kwani ana shida gani? Anaonekana kama… mtoto wa miaka mitatu au minne hivi.

**20. CHEMU** Ni ukoo wao….! wote wana miili nimidogo katika familia yao. Unamkumbuka Dadake shuleni kwetu.. Yule anaitwa Jane? Tuko rika moja lakini anaonekana mdogo sana,hanifikii.

**21. SAM** Unasema yule msichana mrembo, mwembamba hivi na tabasamu nzuri?

**22. CHEMU** ***(angry)*** Si mrembo. Amekonda, na anaumwa kila wakati.Hukosa kuja shuleni mara nyingi.

**23. SAM** ***(apologetic)*** Sawa…! sawa…..! si mrembo vile. Lakini kwanini hukosa kwenda shule kila mara.?

**24. CHEMU** Unakumbuka ulipokuwa ukiugua ugonjwa wa kuhara, na ukakosa kwenda shule kwa muda wa wiki mbili. Yeye kila mara ana haraha na anakosa kuja shule.

**25. SAM** Lakini kwanini asiende kupata matibabu?

**26. CHEMU** ***(angry)*** Sam, fahamu mimi ni mwanafunzi mwenzake sio Mamake!!

**27. SAM** Nilikuwa nikijiuliza tu….. na ninamhurumia sana.!.

**28. CHEMU** ***(angry)*** Kwanini una muhurumia ? Hata humjui na si rafiki yako ….! kwanini umuhurumie?

**29. SAM** *(**apologetic)*** Sahamani Chemu.. wewe ni rafiki yangu lakini si mgonjwa kama yeye..…

**30. CHEMU**NAYOZUNGUMZIA MAS ***(sneering****)* Humjui wewe …ni mzembe,… na goigoi …. Na njii ….…

**31. SAM** Wacha kumsema vibaya mwenzako.

**32. CHEMU** Sam,nakwambia, hata wakati anapokuja shule kila wakati anakuwa wa mwisho katika mitihani.

**33. SAM** ***(shouting)*** Chemu, unamuonea wivu !

**34. *SFX: KID WHIMPERS***

**35. CHEMU** **Angalia** sasa ulichokifanya.

**BRIDGE MUSIC**

**36. NARRATOR** NAAM.. HATA SAM NA CHEMU WANAWEZA KUIONA TOFAUTI YA MTOTO ALIYE NA UMRI MDOGO KINYUME NA KAWAIDA, AU ASIYESHIKA SHULENI.TUSIKILIZE TUPATE KUFAHAMU ZAIDI KWANINI JANE ANACHUKUA MUDA MREFU KUELEWA MASOMO NA KWANINI KWAKU ANA MWILI MDOGO SANA LICHA YA UMRI WAKE..

**SCENE 2: EDITH'S HOME**

**37. EDITH** Eddi na Dkt Sally nashkuru sana kwavile munatujulia hali kila wakati.Kweli wewe ni shemeji anayenijali. Hata wewe Dkt Sally nashukuru juhudi zako licha ya kazi nyingi hospitalini! Hapana shaka Mume wangu, …mungu amrehemu!..... , ambaye ni kakako pia anaridhishwa na juhudi hizi mahali alipo..

**38. EDDI** **Edith**, ni wajibu wetu kuja kuwajulia hali. Hasa baada ya yote yaliyomsibu marehemu Fatu.

**39. EDITH** Mungu ailaze pia roho yake mahali pema peponi.Kwa sasa nina kituo baada ya matokeo ya uchunguzi tuliofanyiwa hivi karibuni**.** Hakuna mtu mwengine atakayeugua ugonjwa wa kuhara katika familia hii tena,hata Sam na Chemu pia. Unajua nilikuwa na wasiwasi tulipokwenda kupimwa.

**40.** **EDDI** Najua ulikuwa na wasi wasi..

**41.** **DR SALLY** Sam anaendeleaje?. Yuko wapi ?

**42.** ***SFX: DOOR BURSTS OPEN. THREE PAIRS OF FOOT STEPS RUSH IN*****.**

**43.** **SAM** Mjomba Eddi,…. Shangazi Sally!.

**44.** **CHEMU** Mjomba Eddi , Dkt Sally!

**45.** **EDDI** Sam na Chemu munaendeleaje sasa ? Hata tulikuwa tukiwazungumzia nyinyi wawili.

**46.** **DR SALLY** *Chemu,* umetuletea mgeni? Huyu ni mtoto wa nani?

**47.** **CHEMU** Anaitwa Kwaku, nimekuwa nikishinda na huyu mtoto wa jirani,na Sam akamuamsha. Ndipo tukasikia mngurumo wa gari lenu

**48.** **EDDI** Ni vizuri sana kushinda na mtoto.

**49.** **SAM** *(**teasing**)* Chemu anamtunza mtoto anayeonekana dhaifu sana.

**50.** **EDITH** Sam, wacha kusema hivyo , si vizuri…….

**51.** **CHEMU** Sam, Lakini si makosa yangu….huyu mtoto anaendelea kuwa mdogo tu licha ya umri wake,…. Kamwe hakui….

**52. EDITH** Na kila nikimuona mtoto huyu anajikuna tu kana kwamba ana viroboto mwilini**.**

**53. DR SALLY** Maskini mtoto ***(To Kwaku)*** Kwaku… Kwaku, njoo hapa mtoto wangu.. hebu nikuangalie.. amenyamaza kana kwamba hawezi kuongea.

**54. SAM** Dr Sally, pia tungemuita Dadake uweze kumfanyia uchunguzi pia. Ni mwembamba sana na ni mgonjwa kila mara

**55. CHEMU** ***(interrupts)*** Si mrembo…. Anahara na pia ana ajizi……hafahamu mambo kwa upesi darasani …...

**56. EDITH** ***(to Sam and Chemu)*** Hebu nyamazeni nyinyi wawili.

**57. DR SALLY** Eddi, angalia, unazitambua hizi alama mwilini mwake ? Uzito wake pia umepungua sana.!

**58. EDDI** Kuna tatizo kubwa hapa.. Kwaku hakui inavyotakiwa!

**59. EDITH** Eddi,jihadhari na kauli zako kumhusu mtoto wa jirani yetu.Huenda tukajikuta matatani!

**60. DR SALLY** Mimi sijali wanayosema majirani, lakini mtoto huyu anahitaji matibabu ya dharura.

**61. CHEMU** Oh ooh … Dkt Sally kweli unaweza kumfanya akue awe mrefu?

**62. DR SALLY** Chemu, Kwaku ni mdogo sana kuliko umri wake. Tunaweza kusema amedumaa.

**63. CHEMU** Lakini kwanini anaendelea kuwa mdogo hivi

**64. EDITH** Chemu, ninahakika Dkt Sally atamshauri Mama Kwaku njia bora za kuiimarisha afya yake.Nadhani sasa Mamake amerejea. Mrudishe lakini mwambie mamake kwamba Dkt Sally anakuja kumuona.

**65.** ***SFX: FOOTSTEPS. DOOR OPENS AND SHUTS.***

**66. SAM** Sasa nini kinachomsumbua?

**67. DR SALLY** Sam, Unakumbuka chango uliokuwa nao tumboni wakati ulipokuwa ukiugua ugonjwa wa kuhara. Kwaku pia ana minyoo, lakini minyoo yake ni tofauti. Ana minyoo aina ya ***TEGU.***

**68. EDITH** Minyoo, mtoto huyu aliipata vipi?

**69.** **EDDI** Edith, Unakumbuka tuliyojifunza awali, kuhusu umuhimu wa kunawa mikono, kuchemsha maji ya kunywa na kuosha chakula? Minyoo hii huishi tumboni. Na ili ikue,lazima ikile chakula kilicho tumboni mwa mtoto huyu..

**70.** **SAM** Oh ooooh inasikitisha! .

**71.** **EDITH** Maskini Mtoto.

**72.** **DR SALLY** Tuseme hivi, minyoo hii hukila chakula kinachopaswa kumsaidia Kwaku kukua vizuri.Tegu pia hujipatia virutubishi kwa kuifyonza damu ya mtoto . Kila mnyoo unafyonza kiasi kidogo.Mtoto aliyeambukizwa anaweza kuwa na tegu wengi sana tumboni mwake, na kadri hali hii inavyoendelea kupuuzwa ndivyo minyoo inavyozidi kuongezeka na athari zake.

**73.** **SAM** Ahhh kweli ….! na watu bado hawajazifahamu njia za kupambana au kuzuia kuambukizwa minyoo. Ni rahisi ***(to himself)*** Lazima tuitafute suluhu ya tatizo hili….

**74.** **EDDI** Mbali na hayo mtoto pia anapata ugonjwa wa kuhara ulio sugu na homa kali.

**75. EDITH** Oohh Eddi..huo ni ugonjwa mbaya sana.Na ngozi yake je… unaona hizi alama za kujikuna kila mahali.

**76. DR SALLY** Hizi ni alama za viluwiluwi vya Tegu...

**77. SAM** ***(interrupts)*** **Viluwiluwi ni nini**?

**78. EDDI** Swali zuri sana . Tunaweza kusema ni minyoo ambayo haijakomaa

**79. DR SALLY** Wakati mtu anapoambukizwa, viluwiluwi hivi….,yaani minyoo ambayo haijakomaa inayopatikana katika mazingira machafu.., hupenya kwa urahisi kwenye ngozi.Baada ya kupenya eneo linakuwa na muwasho na vina acha alama kwenye ngozi. Viluwiluwi hivyo huhamia kwenye mishipa ya damu na vinaweza pia kuivamia koromeo na hata mapafu.

**80. SAM** Yaani …. Viluwiluwi hivi ni kama vinasafiri katika mwili wa binadamu**.**

**81. EDDI** Haswa…. Lakini safari hii huwa na madhara makubwa kwa mwanadamu..

**82. EDITH** Sally, endelea tafadhali… nimeshikwa na hofu..!.

**83.** **DR SALLY** Hatimaye viluwiluwi hivi hufika tumboni na vinabadilika kuwa minyoo

**84.** **SAM** ***(alarmed)*** Dkt Sally,Twende sasa, twende tukampeleke Kwaku hospitali. Kisha tutafute njia ya kuihamasisha jamii nzima kuhusu ugonjwa huu.

**85.** ***SFX: DOOR BURSTS OPEN.***

**86.** **MARIA** **(shouting)** Huyu msichana wangu mvivu yuko hapa?

**87.** **EDDI** Habari za asubuhi Maria. Ni jambo gani la dharura linalokufanya usituamkue asubuhi hii!

**88.** **MARIA** Aaah… samahani, Mumeamkaje nyote.. Asubuhi yangu si nzuri. Chemu yuko hapa?

**89.** **EDITH** Amekwenda kwa Mama Kwaku. Hata sisi pia tunaelekea huko.

**90.** **MARIA** Kwanini? Kwani ghafla Mama Kwaku amekuwa kivutio cha watalii? Ni mama wa kawaida tu wa yule mtoto mbilikimo na msichana mvivu.

**91.** **DR SALLY** Kwaku ana ***Tegu*** na yule mwengine … anaitwa nani jina lake vile?

**92. MARIA** Yule msichana mjinga asiyeelewa kitu? Anaitwa Jane.

**93. DR SALLY** Yeye si kwamba ni mjinga.Ana matatizo.

**94. MARIA** Bila shaka ana matatizo… ni mgonjwa wa akili.

**95. EDITH** ***(exclaiming)*** Maria! Mara nyingine huna huruma kabisa!!

**96. EDDI** Tafadhali tusikizaneni hapa… hili ni suala muhimu sana.

**97. DR SALLY** Jane huenda amekuwa akiishi na tegu hao kwa muda mrefu sana. Haya yote, yaani ugonjwa wa kuhara na minyoo inayofyonza virutubishi mwilini ndio chanzo cha kudumaa na kuwa mvivu.

**98. MARIA** Hakuna tofauti yoyote….yeye ni mvivu na akili yake haifanyi kazi.

**99. EDDI** Natumai athari hizi hazijavuruga mambo

**100. MARIA** Sisi…. Sisi …? Eddi hebu niambie mimi nimechangia vipi hali hiyo?Si kosa langu. Ninachopaswa kufanya, tena haraka ni kwenda nyumbani kwa Mama Kwaku kumuokoa msichana wangu mwerevu asije akaambukizwa hali hiyo ya akili.. Wacheni niende mara moja.

**101. EDITH** ***(shouting)*** Maria! Wewe huna huruma hata kidogo.

**102. DR SALLY** Hata sisi Maria,pia tunaelekea huko nyumbani kwa Mama Kwaku. Watoto wake lazima wapelekwe hospitali mara moja..

**103. MARIA** Sasa mnasubiri nini? Twendeni basi….!.

**BRIDGE MUSIC**

**OUTRO**

**104. NARRATOR** MSIKILIZAJI, HEBU LIFIKIRIE HILI LA KUGAWANA UNACHOKULA NA MAMIA YA MINYOO TUMBONI MWAKO!KUMBE NDIO MAANA KWAKU AMEDUMAA NA AMEATHIRIKA KWA MUDA MREFU. JEE NI WANGAPI KATI YETU WANA MINYOO TUMBONI NA HAWAFAHAMU?

SASA SAM ANATAFAKARI JINSI YA KUWASAMBAZIA WENGINE HABARI HIZI NJEMA. LAZIMA APATE NJIA MUAFAKA YA KUWAELIMISHA WENGINE YOTE AMBAYO FAMILIA YAKE IMEJIFUNZA KATIKA MUDA WA WIKI CHACHE ZILIZOPITA.LABDA WAKATI WATAKAPOKUTANA WOTE WATAFIKIA MAKUBALIANO YA KUZINDUA MPANGO MAALUM.

USIKOSE KUUNGANA NASI TENA WAKATI MWENGINE TUTAKAPOKUTANA KWA MAKALA YA MWISHO YA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO. UKIPENDA KUISIKILIZA TENA MAKALA HII, AU KUTUMA MAONI YAKO, TAZAMA MTANDAO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE KWA MAELEZO ZAIDI. HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.